BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 11 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora :

134. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tunaipongeza Serikali kwa kuongeza mishahara na posho kwa watumishi wa umma, ikiwa ni pamoja watumishi wa kada ya manunuzi ambao hufanya kazi kubwa yenye vishawishi vingi vibaya vinavyoweza kuwaingiza watumishi hawa katika tamaa za rushwa na tamaa ya kupokea ten percent (10%) katika kazi zao, hali ambayo pamoja na sababu nyengine, hutokana na mishahara yao kuwa midogo tofauti na wenzao katika kada ya uhasibu.

(a) Je, ni lini Serikali inafikiria kuwaongezea mishahara na posho watumishi wa kada hii ya manunuzi kama wenzao wa kada ya uhasibu.

(b) Je, ni kiwango gani cha mishahara na posho hulipwa watumishi hawa wa kada hizi mbili katika nafasi zote za kiutumishi kwa mujibu wa elimu zao.

(c) Je, tathmini inaonyesha ni kiwango gani cha watumishi waliosomea fani ya manunuzi imeajiriwa na vipi wanakidhi lengo la mahitaji ya taasisi zetu.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

20. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali katika kujenga miundombinu tofauti mjini na vijijini, bado kuna changamoto katika baadhi ya maeneo kujaa na kutuwama kwa maji kutokana na kutokuwepo mitaro. Hali kama hiyo inajitokeza katika shehia ya Mbweni maeneo ya Kisima Mbaazi, Mbweni Kibokoni, shehia ya Michungwani na baadhi ya maeneo ya Kiembesamaki.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondosha kadhia hiyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

270. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

(a) Je, ni kwa nini panapokuwepo na nyongeza ya bajeti katika miradi ya maendeleo au kuwepo haja ya kuanzishwa miradi ambayo hapo awali haikupitishwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kunakuwa hakuna maombi ya bajeti ya ziada katika Baraza hilo.

(b) Je, katika mradi wa uboreshaji wa Uwanja wa Amani, kulitumika utaratibu gani wa kibajeti kwa vile haukuwemo katika Bajeti iliyopitishwa na Baraza.

(c) Kwa kuwa katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa masoko na baadhi ya barabara, gharama zake halisi zilizidi kwa kiasi kikubwa cha fedha zilizopitishwa na Baraza, na kwa kuwa kitendo cha kutokuomba bajeti ya ziada kwa miradi hiyo hupelekea kuvunjwa vifungu vya Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, je, ni upi utaratibu sahihi wa kutorudia makosa hayo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

117. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali iliamua kuitengeneza Meli ya MV. Mapinduzi II kwa lengo la kuimarisha huduma za usafiri kwa wananchi na kupunguza changamoto za usafiri zinazowakabili. Licha ya nia hii njema, kumekuwa na malalamiko kuhusu uamuzi huo wa Serikali kwa sababu awali meli hii ilikuwa katika mpango wa kuuzwa.

(a) Je, ni sababu gani za kitaalamu zilizopelekea meli hii kutouzwa na badala yake kurudishwa katika mpango wa Serikali wa kuitengeneza.

(b) Je, ni lini meli hii itamaliza matengenezo na kuanza tena kutoa huduma kwa wananchi.

(c) Je, ni gharama za kiasi gani zitakazotumika katika ukarabati wa meli hii, ili kuiwezesha kuendelea na kutoa huduma, na ni upi mpango wa Serikali wa muda mrefu wa meli hiyo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

146. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili, Mifugo:

Pamoja na uingizaji mkubwa wa ng’ombe na wanyama wengine ambao huchinjwa kwa matumizi ya kitoweo hapa Zanzibar kwa kila mwaka, machinjio yetu yanayotumika kufanyia shughuli hizo kwa muda mrefu yamebaki katika hali mbaya, jambo ambalo ni hatari kwa matumizi ya watu wetu.

(a) Je, kivipi Serikali inalitambua tatizo hili.

(b) Je, Serikali imewahi kufanya tathmini yoyote ya kitaalamu juu ya machinjio ya Kisakasaka na hali yake iko vipi.

(b) Je, ni upi mkakati wa haraka wa Serikali katika kuhakikisha machinjio yetu haya, hayahatarishi maisha ya watumiaji wa nyama.

234. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Taratibu za kisheria na kikanuni ziko vipi kwa watu wanaowadhalilisha, kuwanyanyasa, kuwapiga, kuwatesa, kuwabeza, kuwajeruhi na kuwatoa uhai wanyama wao bila ya kibali au ruhusa kutoka kwa mamlaka husika.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

139. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kumekuwa na malalamiko ya wananchi wa kijiji cha Daya, jimbo la Mtambwe ambao waliomba viwanja katika shamba la Serikali liliopo katika eneo la Daya kwa Mjinga. Baada ya kukaa kwa muda mrefu bila ya kupatiwa majibu, inasemekana eneo hilo limetolewa kinyume na utaratibu na kupewa mtu mwengine wa nje ya jimbo la Mtambwe ambae ameanza kuuza viwanja kinyume na utaratibu.

(a) Je, Serikali inalifahamu jambo hili ambalo tayari limeleta sura ya mgogoro katika eneo hili.

(b) Je, ni upi utaratibu wa kutoa maeneo ya mashamba ya Serikali ambayo hayana miti kwa wananchi kwa ajili ya kujenga nyumba za kuishi.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

75. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuunda 'TASK FORCE' kwa ajili ya kupambana na magendo ya karafuu. Hata hivyo, juhudi hizo bado hazijaleta tija iliyokusudiwa kutokana na vitendo hivyo vya magendo vinavyoendelea siku hadi siku.

Je, Serikali ina mpango mwengine madhubuti wa kukabiliana na jambo hili la magendo.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

32. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Hapo nyuma, Serikali ilianzisha utaratibu wa kuwapatia madaftari ya kuandikia wanafunzi wote wa skuli za msingi na sekondari lakini kwa sasa utaratibu huu umesita.

    Je, kuna sababu gani zilizochangia kusita kwa utararibu huo.

236. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) -Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Ni kwa kiasi gani ujio wa maboresho ya mitaala mipya ya elimu, utakidhi kiu ya kupata wanafunzi wenye uwezo wa kutafakari na kudadisi badala ya ule wa kuwatayarisha kwa ajili ya kupata "grade" za juu tu.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

185. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Bado kuna muamko mdogo kwa wananchi juu ya elimu ya usalama wa chakula, pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuwaelimisha huko.

    (a) Kwa kuwa bado upo umuhimu wa kuwaelimisha wananchi wetu, Je, ni maradhi gani yanayosababishwa na kutokuwepo kwa usalama wa chakula hapa Zanzibar.

    (b) Ni rika lipi la watoto linaloathirika zaidi na tatizo hili.

    (c) Kwa kuwa ni maradhi yanayoweza kuepukika, ni upi mpango wa Wizara wa kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ikiwa ni pamoja na wapishi na wafanyabiashara mbali mbali wa vyakula hapa Zanzibar.

212. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Watu wengi hawana utamaduni wa kupima afya zao, jambo ambalo lina athari kubwa kwenye ongezeko la maradhi mbali mbali.

Je, Wizara yako inatumia utaratibu na mikakati gani ya kutoa hamasa ya elimu ya kupima afya kwa wananchi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

226. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

(a) Ni taasisi ngapi na ni zipi zinazojishughulisha na masuala ya tafiti katika sekta ya utalii Zanzibar.

(b) Ni tafiti zipi ambazo zinasaidia kutoa miongozo na masuluhisho chanya katika kutatua changamoto mbali mbali za Sekta ya Utalii Zanzibar.

**Zanzibar,**
**11 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**